| Huduma zetu | Jukumu la mteja | Kiwango cha huduma | Ada ya huduma |
|---|---|---|---|
| **Huduma za Fedha na uhasibu** | | | |
| 1. Malipo kwa wagawaji na waelekezi wa huduma | • Kuwasilisha mizigo na huduma au kazi kama ilivyo katika mkataba<br>• Wasilisha Ankara/bili | Kulipia uwasilishaji wa bidaa/huduma au kazi kati ya majuma mawili baada ya kuwasilisha ankara/bili au cheti. | Bure |
| **Uteuzi na Uajiri** | | | |
| Kutayarisha maombi ya kazi | • Kuitikia matangazo kwa kuomba kazi<br>• Kuwasilisha stakabadhi zinazohitajika | Kuwajulisha wateuliwa kati ya mwezi mmoja baada ya tarehe ya makataa | Bure |
| Uteuzi wa wafanyikazi | Kuhudhuria mahojiano kama ilivyopangwa | • Kufanya mahojiano kwa usawa, bila mapendeleo na kwa<br>• kuzingatia maadili Kuwajulisha waliofuzu kati ya majuma 2. | Bure |
| **Mawasiliano** | | | |
| Kuitikia simu | • Heshima<br>• Kujitolea kutoa habari zinazotakikana | • Pokea simu kati ya milio mitatu na kuitikia maombi kati ya dakika 3. | Bure |
| Kushughulikia barua na barua pepe | • Kutoa anwani sahihi<br>• Mawasiliano yaliyosawa | Kuitikia kikamilifu kati ya juma moja kwa barua na kati ya siku mbili kwa barua pepe. | Bure |
| Kushughulikia wageni | Heshima na ushirikiano | Usikivu, heshima, staha na kuitikia kikamilifu kati ya dakika kumi punde wanapowasili. | Bure |

## Kwa habari zaidi wasiliana na:


**Mkurugenzi**
Kituo cha Kitaifa cha Utafiti wa Jinai
Jumba la NSSF Orofa ya 19, Bloku A, Sehemu ya Magharibi
SLP 21180-00100
NAIROBI
Simu 254-020-2716762/64
Barua Pepe: ncrckenya07@gmail.com


# KITUO CHA KITAIFA CHA UTAFITI WA JINAI

# MKATABA WA HUDUMA

Mei 2013

## Utangulizi

Kituo cha kitaifa cha uchunguzi wa jinai (NCRC) ni shirika la kitaifa chini ya Afisi kuu ya Sheria kilichoanzishwa na uchunguzi wa jinai kifungu cha 62 katika sheria za Kenya.

Kituo hiki kina halmashauri ya utawala yenye mamlaka ya kuunda sera za utafiti na utaratibu wa kituo.

Mkurugenzi ndiye afisa mkuu mtekelezaji vile vile katibu katika halmashauri ya utawala.

## Jukumu Letu

Jukumu letu ni kufanya utafiti kulingana na chanzo cha jinai na kinga zake na kusambaza matokeo ya utafiti na maoni kwa mawakala wa kiserikali wanaohusika na haki za jinai na washikadau wengine.

## Ruwaza

Kuwa taasisi maarufu ya utafiti wa jinai ulimwenguni.

Ujumbe wetu

Kutoa utafiti bora na thabiti wa sabau za jinai na kinga zake kwa mtazamo wa kuwa na jamii isiyokuwa na jinai.

## Kiini cha thamani yetu

- Weledi na kazi ya pamoja
- Kulenga wateja
- Uongozi wenye ushauriano
- Uwazi na uwajibakaji
- Imani na uaminifu
- kujenga uhusiano wa kudumu
- Wajibu wa kijamii

## Shughuli Zetu Muhimu

(a) Tunafanya utafiti unaoratibiwa katika mipango inayofatilizwa na mawakala wanaohusika na utawala wa haki za kijinai.

(b) Tunafanya utafiti kwa chanzo cha jinai na kinga zake katika sehemu zifuatazo:

(i) Kundi au uhalifu unaohusiana na utamaduni
(ii) Uhalifu unaohusiana na siasa za kijamii na uchumi vile vile ulanguzi wa mihadarati, magendo ya binadamu, kuchuuza au kutawaliwa.
(iii) Njia ya utendaji kwa watu wanaojihusisha na uhalifu wa aina yeyote.
(iv) Uhalifu wa vijana
(v) Mikengeuko iliyoko kutoka kwa mfumo wa haki za kijinai katika kuongeza uhamasisho wa jukumu la jamii katika kurekebisha wahalifu.

(c) Tunasambaza matokeo ya utafiti na mapendekezo kwa mawakala wa serikali wanaohusika na utawala kwa haki za kijinai na washikadau wengine kupitia uchapishaji, warsha, semina, vifaa vya usambazaji habari na njia nyingine mahususi.

## Wateja Wetu

Mkataba huu wa huduma unajumuisha mawakala wa serikali wanaohusika na utawala wa haki za kijinai, taasisi za elimu, waendelezaji wenza na washiriki wengine katika taasisi za utafiti na washikadau wengine wakuu.

## Kanuni za Huduma Zetu,

Tunajitolea kwa haya yafuatayo:-

- Kuhudumia wateja kwa heshima, ustahifu na taadhima.
- Kutoa kwa upesi habari sahihi punde zinapotakikana.
- Kuweka mbele umuhimu wa kituo, wateja na umma kwa mumla bila kujali ubinafsi.
- Kushughulikia mahitaji ya wateja kwa usiri na kwa haraka kama inavyostahili.

## Kuangalia upya mkataba wa Huduma

Kwa kuzingatia mabadiliko katika matarajio ya wateja wetu tunajitolea kuangalia upya mkataba wa huduma mara moja kwa mwaka kwa kushauriana na wateja wetu na washikadau wengine husika. Haya yote yatafanywa ili kuhakikisha wendelezaji wa ubora wa huma kwa wateja wetu.

## Mwitiko

Ili kutusaidia kila wakati kuendeleza huduma zetu, tunakubali malalamishi, wasifu mapendekezo kwa kutumia kisanduku chetu cha mapendekezo. Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa kutumia anwani iliyoko hapa. Vile vile kila mwaka tunakagua na kutathimini uradhi wa wateja wetu.

| Huduma zetu | Jukumu la mteja | Kiwango cha huduma | Ada ya huduma |
|---|---|---|---|
| **Huduma za utafiti** | | | |
| 1. Kufanya utafiti wa jinai tunapoulizwa na wakala | • Ombi kwa maandishi au kumbukumbu za ulewano<br>• Kuzingatia kanuni na utaratibu<br>• Kupeana habari ili kurahisisha utafiti | • Tunajulisha mteja kwamba tumekubali au tumekataa maombi katika mda wa mwezi mmoja.<br>• Kufanya utafiti unaohitajika kulingana na mwongozo wa utafiti na maadili | Kulingana na makubaliano na masharti ya mkataba |
| 2. Kufanya utafiti wa kuwaida na kusambaza matokeo kueleza sera | Kupeana habari ili kurahisisha utafiti | Kufanya utafiti na kushughulikia uhalifu uliopo na ulipokithiri kulingana na mwongozo wa utafiti na maadili | Bure |
| 3. Kusambaza matokeo kwa utafiti na habari nyingine. | • Maombi kwa maandishi<br>• Kujitambulisha | Kutoa maandiko katika kituo cha rasilimali kwa muda wa dakika (20) kama yako katika maeneo hayo na kwa siku moja kama yako kwingine. | Kama ilivyo katika maandiko. |